

**HOTUBA YA MGENI RASMI NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA  
UCHUKUZI MHE. MWITA WAITARA (MB) KATIKA UZINDUZI WA  
TOVUTI YA BARAZA LA USHAURI LA WATUMIAJI WA HUDUMA  
ZA USAFIRI ARDHINI (LATRA CCC) TAREHE 01 OCTOBER 2021**

**MH. Amos Makala - Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam,  
Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya ya Temeke, Kigamboni, Ilala,  
Kinondoni na Ubungo,  
Wakuu wa taasisi mbalimbali za Serikali na sekta binafsi,  
Wajumbe wa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za  
Usafiri Ardhini,  
Wawakilishi wa Majukwaa ya Wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha  
Dar es Salaam,  
Wawakilishi wa Vilabu vya Wanafunzi wa Sekondari na Shule za  
Msingi za Mkoa wa Dar Es Salaam;  
Wageni waalikwa,  
Sekretarieti ya Baraza,  
Wanahabari,  
Mabibi na mabwana.**

Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai na kwa kutujalia neema ya kukutana hapa kwa ajili ya uzinduzi wa tovuti ya Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini. (LATRA CCC). Baraza hili lipo kwa mujibu wa Kifungu Namba 29 (2) cha Sheria namba 3 ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, (LATRA) ya Mwaka 2019.

**Ndg, Wageni Waalikwa,**

Nataka kuwajulisha Majukumu ya Baraza kama ilivyo katika sheria kuwa ni:

- (i) Kuwakilisha maslahi ya watumiaji wa huduma za usafiri Ardhini, kwa kuwasilisha, kupata maoni na taarifa na kwa kushauriana na Mamlaka, Waziri mwenye dhamana na wadau wa sekta mbalimbali zinazodhibitiwa;
- (ii) Kupokea na kusambaza taarifa na maoni mbalimbali kuhusu masuala yanayowagusa watumiaji wa huduma zinazosimamiwa na LATRA;
- (iii) Kuunda kamati za Watumiaji wa huduma za usafiri wa Sekta zinazodhibitiwa na LATRA katika Mikoa na Kushauriana nazo;
- (iv) Kushauriana na wadau , Serikali na makundi ya watumiaji kuhusu huduma;
- (v) Kuunda mabaraza ya Watumiaji wa huduma za Usafiri Ardhini, kwenye maeneo ya Jamii na Kushauriana nazo;
- (vi) Kufanya utafiti juu ya maslahi, haki, wajibu na masuala mengine yanayogusa watumiaji.

Aidha, utekelezaji wa Majukumu haya yanapaswa kuzingatia misingi ya Sheria, Kanuni na miongozo mbalimbali, inayotolewa na Serikali mara kwa mara.

Nafarijika kusikia, utengenezaji wa emails na tovuti ya Baraza umefanywa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) **Hongereni sana**

**Ndg, Wageni Waalikwa,**

Kama mlivyosikia kwenye taarifa ya utendaji wa Baraza, kuwa Baraza limefanikiwa:

- (1)Kutoa elimu kwa abiria juu ya kujikinga na Maambukizi ya COVID 19 kwenye Vyombo vya Usafiri wa Umma.
- (2)Kutoa elimu kwa abiria juu ya kukata tiketi kwa njia ya mtandao;
- (3)Kuelimisha abiria juu ya haki na wajibu wao,
- (4)Kuhamasisha abiria wa Kituo Cha Mabasi cha Mbezi kupanda magari kwa kukaa kwenye Mstari.

Lakini bado Sekta hii, inakabiliwa na changamoto kadhaa.

**Ndg, Wageni Waalikwa,**

Sekta hii ya Usafiri Ardhini inakabiliwa na changamoto kadhaa zinazoathiri watumiaji wa Huduma kama ifuatavyo:

- (a) Kuongozeka kwa ajali za Babarani. Tatizo hili ni kubwa kwani limeendelea kuua mamia ya watumiaji wa vyombo vya Usafiri barabarani;
- (b) Abiria kukosa fursa ya kukata tiketi kwa njia ya mtandao;
- (c) Abiria wa Mijini kuingia kwenye vyombo vya Usafiri kwa fujo, jambo ambalo limeathiri saikolojia ya Watoto, Wazee, akinamama wajawazito na makundi mengine;
- (d) Kuongezeka kwa misongamano ya magari mijini;
- (e) Kuwepo kwa migogoro mingi kati ya abiria na watoa Huduma n.k

Hali hizi zote, zinafanya Sekta hii, inayohudumia zaidi ya asilimia 90 ya Watanzania, kuwa na kiwango cha chini katika

Huduma au kukosa uwiano kati ya matarajio ya Mteja (abiria) na Mtoa huduma za Usafiri.

**Ndg, Wageni Waalikwa,**

Tumesikia kilio cha watumiaji wa Huduma hizi za Usafiri zinazosimamiwa na taasisi mbalimbali za Serikali, zikiwepo LATRA, Jeshi la Polisi, Vyuo vya Ufundishaji madereva na Wadau wengine, changamoto hizi zinazoathiri watumiaji wa Huduma Chanzo chake ni nini?

- (a) Kuongozeka kwa ajali za Babarani, zinazosababishwa na mwendo kasi. Pamoja na Serikali kuwa na nyenzo nyingi za udhibiti kama VTS, kwa nini usimamizi wake unakuwa mgumu? Tunafeli wapi? Abiria wanaendelea kupoteza maisha.
- (b) Abiria kukosa fursa ya kukata tiketi kwa njia ya mtandao; Tatizo lipo wapi?
- (c) Abiria wa Mijini kuingia kwenye vyombo vya Usafiri kwa fujo, wengine kupita madirishani, hii ni fedheha kubwa;
- (d) Kuendelea kuwepo kwa migogoro mingi kati ya abiria na watoa Huduma haileti afya kwa abira wetu. Tukumbuke Msemo usemao, Mteja ni Mfalme/ Malkia. Je? Mteja wa Huduma za Usafiri ni Mfalme/ Malkia kweli? Au ni **mhanga wa Huduma?**

**Niwaombe viongozi wote mliopo hapa na wengine, kushirikiana na Baraza, linalowakilisha maoni ya Watumiaji, kuona ni kwa namna gani ya kutatua changamoto hizi zinazolalamikiwa na Watumiaji wa vyombo vya Usafiri Nchini.**

**Ndg, Wageni Waalikwa,**

Katika Dunia ya sasa, ili kuweza kufikia maendeleo ya kweli, ni lazima kutumia nyenzo za teknolojia ili kuweza kuufahamisha umma, unachokifanya na wewe uweze kujifunza kwa wenzako wanachokifanya. Hivyo Baraza kuwa na TOVUTI ni chombo muhimu sana katika mawasiliano.

Kama tulivyoona, tovuti hii imetengenezwa kwa umahiri mkubwa na Wataalamu wetu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao, na imezingatia mahitaji yote ya Serikali, kwa kuonyesha, historia ya baraza, dira na dhamira, majukumu, msingi mkuu, muundo wa taasisi, vipeperushi, makala, sheria na kanuni, majarida, sera na elimu kwa mtumiaji wa huduma za usafiri ardhini kwa ujumla. Nawashukuruni sana eGA kwa kazi hii nzuri mliyoifanya.

**Hongereni sana.**

**Ndg, Wageni Waalikwa,**

Ni kwa kutumia tovuti hii, [www.latraccc.go.tz](http://www.latraccc.go.tz) kuweza kuuhabarisha umma, juu ya Majukumu, kazi na Mipango yenu ya kutatua changamoto mbalimbali zilizopo katika Sekta hii.

Miongoni mwa mipango mliyoeleza kuwa ni:

1. Kuhimiza zaidi matumizi ya tiketi mtandao na smart cards kwa vyombo vyote vya Usafiri,

2. Kuelimisha abiria juu ya haki na wajibu wao, hasa kukemea vitendo hatarishi kwenye vyombo vya Usafiri, ikiwemo mwendo kasi,
  3. Kuhamasisha abiria kuingia kwenye mabasi ya Mijini kwa Mstari pamoja na mipango mingine;
- Niwahakikishie, Mimi kama Naibu Waziri Mwenye Dhamana na Sekta hii, ninaunga mkono jitihada zenu, na Sote kwa Pamoja tuunge Mkono Jitihada za **Mh. Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania** **Mh. Samia Suluhu Hasan** katika kuendeleza maendeleo ya Sekta ya Usafirishaji Nchini, kwa Manufaa ya Wananchi wote.

**Ndg, Wageni Waalikwa,**

Kwa heshima kubwa, Mh. Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Wakuu wa Wilaya zote za Mkoa wa Dar es Salaam, Viongozi mbalimbali mliopo hapa pamoja na Jamii yote ya Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini, niwaombe, tuunge mkono jitihada hizi za Baraza ambayo zimebekwe kwenye TOVUTI tunayoizindua leo ili iwasaidie Watanzania kujua HAKI na WAJIBU wao katika Sekta hii Muhimu ya Usafiri wa Umma.

**Mwisho kabisa natamka rasmi, kuwa tovuti hii;**

**[www.laatracc.go.tz](http://www.laatracc.go.tz) nimeizindua Rasmi.**

**Wote nawatakieni kila la kheri katika kutekeleza majukumu yenu, Asanteni Sana.**